

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA HAMSINI NA MOJA

21 JUNI, 2024



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA HAMSINI NA MOJA TAREHE 21 JUNI, 2024

I. DUA:

II. MASWALI:

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**651. MHESHIMIWA SEIF KHAMIS SAID GULAMALI (MANONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itazipandisha hadhi Shule za Sekondari Manonga, Seif Gulamali, Simbo na Nkinga kuwa za Kidato cha Tano na Sita.

**652. MHESHIMIWA VITA RASHID KAWAWA (NAMTUMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa nyumba za Walimu wa Sekondari nchini na kukarabati zilizochakaa.

**653. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni hatua gani zinachukuliwa ili kupunguza changamoto ya Walimu katika Shule za Msingi na Sekondari Mkoani Mara.

**654. MHESHIMIWA SHALLY JOSEPHA RAYMOND (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kujenga mitaro ili kuzuia uharibifu wa Barabara unaosababishwa na mvua katika maeneo ya milimani Mkoani Kilimanjaro.

**WIZARA YA NISHATI:**

**655. MHESHIMIWA NUSRAT SHAABAN HANJE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Vijiji vyote vya Mkoa wa Singida vitaunganishiwa umeme.

**656. MHESHIMIWA EDWIN ENOSY SWALLE (LUPEMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme wa REA kwenye Vitongoji vya Jimbo la Lupembe.

**657. MHESHIMIWA PROF. PALAMAGAMBA JOHN AIDAN KABUDI (KILOSA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itajenga *Sub-station* ya umeme katika eneo la Dumila - Kilosa.

**WIZARA YA KILIMO:**

**658. MHESHIMIWA PROF. PATRICK ALOIS NDAKIDEMI (MOSHI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itarejesha utoaji wa Ruzuku ya pembejeo za dawa kwa Wakulima wa Kahawa.

**659. MHESHIMIWA STELLA SIMON FIYAO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na ongezeko la bei ya pembejeo za kilimo.

**660. MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN ASENGA (KILOMBERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kati ya Mwaka 2021 – 2022 Serikali ilianzisha miradi mingapi mipya ya umwagiliaji ili kukuza kilimo cha mpunga katika Jimbo la Kilombero.

**WIZARA YA UCHUKUZI:**

**661. MHESHIMIWA JACQUELINE NGONYANI MSONGOZI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanza kujenga Reli ya Mwendokasi ya kutoka Mtwara hadi Mbamba Bay.

## **WIZARA YA FEDHA:**

### **662. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMEDI KUCHAUKA (LIWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, lini Serikali itairejeshea Halmashauri ya Liwale fedha za Miradi ya kimkakati iliyorudishwa Hazina ili iweze kujenga Stendi ya Kisasa.

### **III. HOJA ZA SERIKALI:**

#### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupidisha Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2023 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

#### **WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupidisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
21 JUNI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, ndc  
KATIBU WA BUNGE**